# MSAADA WETU UNATOKA KWA BWANA
## Zaburi 120

Siku ya Mungu ya makumi mawili na kenda ya mwaka C

**M : Bienfait Bisimwa**




1. Ninainua macho yangu nitazame milima;
msaada wangu uta toka wapi?
Msaada wangu unatoka kwa Bwana,
aliye fanya mbingu na dunia.

2. Asiache mguu wako uteleze,
asisinziye anayekulinda.
Kweli, hatasinzia wala hatalala usingizi,
Mlinzi wa Israeli.

3. Bwana ni mlinzi wako,
ukingo wako Bwana kuumeni kwako.
Mchana jua halita kuchoma,
wala mwezi usiku.

4. Bwana atakukinga na uovu wowote,
atalinda roho yako.
Bwana atakulinda unapotoka na unaporudi,
tangu sasa na hata milele.